JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA
Tovuti: www.hlpc.go.tz
Simu: 0750059900 Barua Pepe:hlpc@afya

# TAARIFA KWA UMMA

## KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI OKTOBA 2025

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa Shahada ya Maabara ya Afya ya Binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa tarehe **10.10.2025** Saa **4:00 Asubuhi** na kufungwa **12.10.2025 Saa 4.00 Asubuhi.** Aidha, Maombi yatafanyika kupitia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale walioomba usajili wa awali (Provision registration) baada ya kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni au cheti cha uthibitisho kutoka TCU kwa waliosoma vyuo vya nje ya nchi.

2. Waombaji wote wahakikishe maombi yao yamefanyiwa kazi kwa kufuatilia hatua za maombi hayo kwenye mfumo. Aidha, ili kujihakikisha maombi yako yamekubaliwa lazima angalau upate ujumbe wa **maombi yako kuthibitishwa (*APPROVED*).** Ikiwa maombi yako hajadhibitishwa, utakwama kuchagua kituo cha utarajali.

3. Waombaji wote wanasistizwa kufanya maombi kwa wakati na ikitokea mwombaji atahitaji kubadili kituo cha utarajali itampasa kutumia mfumo wa ***hprs.mo.go.tz*** kupitia akaunti yake. Pia kituo kikiwa hakina nafasi huwezi kuhamia. Aidha zoezi hili la kubadili kituo linatakiwa lifanyike kabla ya dirisha la maombi kufungwa baada ya hapo **HAKUTAKUWEPO NA UWEZEKANO** wa kubadili kituo cha utarajali tena.

4. Aidha, Wote watakaopangiwa vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara kwa tarehe itayaotolewa baadaye ili kuchukua barua na mahitaji mengine ya kwenda mafunzo.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
03.10.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
03 OCT 2025
P.O.Box 743
DODOMA